MAFUNZO YA ZIADA YA KUSOMA KWA UFAHAMU

MWONGOZO WA MWEZESHAJI

Februari 2015

PROGRAMU YA ELIMU YA MSINGI YA TZ2

Shukrani

Mafunzo haya ya kutafakari usomaji kwa walimu wa darasa I na II ni matokeo ya msaada wa watu wa Marekani kupitia ufadhili wa Shirika la Misaada ya Kimataifa ya Maendeleo la Marekani (USAID) kwa Programu ya Elimu ya Msingi ya TZ21. Msaada huu wa watu wa Marekani unalenga kujenga uwezo wa watoto wa Tanzania kielimu. Msaada huu unakusudia kuboresha stadi za usomaji za wanafunzi katika hatua za awali wanapoanza kusoma shuleni ili kuinua matokeo mazuri ya usomaji yanayotarajiwa kwa watoto wote wa shule za Mtwara na Zanzibar. Programu ya Elimu ya Msingi ya TZ21 inatambua mchango wa kipekee uliotolewa na Amy Pallangyo-Mtaalam Mshauri wa TZ21 katika kutayarisha mwongozo huu wa mafunzo. Pia shukrani ziwaendee wafanyakazi wataalamu wa TZ21 na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (WEMU) kwa kuendesha mafunzo ya wawezeshaji wa mafunzo ngazi ya wilaya kwa mkoa wa Mtwara na Zanzibar.

Hivyo basi shukrani za pekee zinatolewa kwa USAID kwa kufadhili kazi hii.

Utangulizi

Mafunzo haya ya ziada ya kusoma kwa ufahamu kwa walimu wa darasa la I na II katika shule za msingi ni juhudi nyingine tena za Programu ya TZ21 kuboresha ufundishaji wa kusoma kwa ufahamu.

Mafunzo haya yanalenga kuimarisha uwezo wa walimu katika kufundisha kipengele cha kusoma kwa ufahamu kwa umahiri mkubwa na wenye kina zaidi.

Madhumuni/viwango vya mafunzo haya ya ziada kwa walimu ni kuwawezesha:

1. Kujua umuhimu wa kufundisha kipengele cha kusoma kwa ufahamu
2. Kujua aina mbalimbali za masomo ya kusoma kwa ufahamu
3. Kujua vipengele vitakavyofanikisha somo la kusoma kwa ufahamu
4. Kupanga jinsi ya kufundisha somo la ufahamu darasani
5. Kufanya mazoezi ya kufundisha masomo ya kusoma kwa ufahamu
6. Kufanya azimio la kufundisha kusoma kwa ufahamu

Ratiba ya Mafunzo

Mafunzo ya walimu wawezeshaji yamepangwa kwa siku 2 kama ifuatavyo:

SIKU YA 1	
Muda	**Shughuli**
2:00 – 3:00	Kujisajili na vifaa
3:00 – 4:00	Ukaribisho, Kujitambulisha, Maelezo ya Jumla kuhusu Mafunzo, Kutafakari Usomaji
4:00 – 4:30	Maduara ya Socrates – Majadiliano ya Kutafakari Ufundishaji
4:30 –5:00	**Chai/Kahawa**
5:00 – 7:00	Usuli wa Usomaji- Majadiliano na Kujifunza
7:00 – 8:00	**Chakula cha Mchana**
8:00 – 9:30	Misingi ya Kufundisha Kusoma kwa Ufahamu
9:30 – 10:00	Maoni na ufupisho wa mafunzo tuliyopata
SIKU YA 2	
2:30 – 3:00	Kujisajili
3:00 – 4:30	Kuchunguza masomo ya mfano
4:30 – 5:00	**Chai/Kahawa**
5:00 – 6:30	Kutayarisha masomo 2 yaliyounganika
6:30 – 7:30	**Chakula cha Mchana**
7:30 – 9:30	Kuonyesha jinsi ya kufundisha somo kwa mwenzako
9:30 – 10:00	Tafakari ya kufunga na maazimio

Vifaa:

1. Kitini cha Kusoma kwa Ufahamu (nakala moja kwa kila mshiriki)
2. Majarida
3. Vifaa vya kuandikia (kalamu na daftari)
4. Projekta, kompyuta, uwasilishaji kwa kutumia kumpyuta na projekta
5. Chati ya karatasi
6. Kalamu za wino mzito za kuandikia kwenye chati
7. Mfano wa Andalio la Somo (nakala 3 kwa kila mshiriki)
8. Sampuli za vitabu vya mwanafunzi kwa ajili ya kutayarisha somo na kufanya mazoezi

Yaliyomo

ukurasa

Shukrani i
Utangulizi ii
Ratiba ya Mafunzo iii
SIKU YA 1 1
Somo la 1: Ukaribisho, Utambulisho, Maelezo ya Jumla Kuhusu Mafunzo, Kutafakari Usomaji 1
Somo la 2: Maduara ya Sokratesi 2
Somo la 3: Kujenga Usuli wa Maarifa 4
Somo la 4: Misingi ya Ufundishaji wa Kusoma kwa Ufahamu 6
Somo la 5: Mhutasari na Kushirikishana Tulichojifunza 7
SIKU YA 2 8
Somo la 6: Kuchunguza Sampuli za Masomo 8
Somo la 7: Kutayarisha Masomo Mawili Yaliyounganika Pamoja 10
Somo la 8: Kufundisha Wenzako Somo 11
Somo la 9: Kufunga 12

SIKU YA 1

Somo la 1: Ukaribisho, Utambulisho, Maelezo ya Jumla Kuhusu Mafunzo, Kutafakari Usomaji (dakika 60)

Vifaa: Daftari la kuandikia, vifaa vya kuandikia, ratiba ya washiriki, chati ya karatasi, kalamu za wino mzito za kuandikia kwenye chati, na projekta

Malengo ya somo la 1: Kujua malengo, matarajio na mchakato wa mafunzo

Muda	Shughuli ya Mwezeshaji	Shughuli za Mwalimu
Dakika15 **Ukaribisho na utambulisho**	Kukaribisha na kutambulisha walimu kutoka katika kila shule. Walimu wote wasimame unapotaja shule zao. Kutambulisha wawezeshaji wengine kwa Mgeni Rasmi kama yupo Kutoa utaratibu wa mafunzo 1. Mazingira ya mafunzo 2. Kuhusu malipo 3. Kuhusu vifaa na rasilimali zitakazotumika Kusimamia mapendekezo ya taratibu/kanuni za kuendesha mafunzo wanazojiwekea Kuandika kwenye chati taratibu na kanuni zilizokubalika na kuzibandika ukutani zionekane kwa walimu wote na kuzifuata.	Walimu husika wasimame wote pindi shule yao inapotajwa Kumsikiliza mwezeshaji Kupendekeza utaratibu na kanuni za mafunzo
Dakika 15 **Kupitia ratiba ya siku mbili na viwango vya mafunzo**	Kuwagawia walimu ratiba ya siku mbili iliyorudufiwa. Kuwaongoza walimu pamoja na washiriki wote kupitia ratiba. Kuwasilisha viwango/madhumuni ya mafunzo Kutoa nafasi ya maswali kama yapo na kuyajibu au kuyabandike ukutani ili yajibiwe baadaye.	Kuchunguza ratiba na kusikiliza mapitio ya ratiba na kuuliza maswali waliyonayo.

Dakika 30 **Kutafakari ufundishaji**	Kuwezesha mchakato wa kuandika kwa kutafakari. Wakumbushe washiriki kuwa tafakari hii ni muhimu sana ili kujenga jukwaa la kubadilishana ujuzi mpya. Maswali yako kwenye wasilisho kwenye projekta au andika maswali haya kwenye chati.	Kujibu maswali haya kwa kuandika *Eleza mbinu unazotumia kwa sasa kufundisha kusoma. Ni kitu gani unakifanya vizuri na kitu gani unakifanya vibaya katika kufundisha kusoma? Ni kwa kiasi gani wanafunzi wako wanajua kusoma vizuri?*

Somo la 2: Maduara ya Sokratesi (Dakika 90)

Vifaa: Chati, kalamu za wino mzito za kuandikia kwenye chati na projekta

Malengo ya somo: Mwalimu aweze:

1. Kutafakari kwa usahihi na uwazi kuhusu aina na ubora wa ufundishaji wao wa sasa wa usomaji
2. Kubainisha maeneo yenye ugumu na kuyaelezea kwa ufasaha
3. Kueleza jinsi mafunzo haya ya siku mbili yatakavyowasaidia kukabili maangaiko yao ya kufundisha usomaji

Muda	Shughuli ya Mwezeshaji	Shughuli za Mwalimu
Dakika 5 **Utangulizi**	**Kuanzisha Somo**: Elezea Maduara ya Sokratesi **Mada**– Majadiliano ya Usomaji **Shughuli:** Kushiriki katika majadiliano katika Maduara ya Sokratesi Elezea malengo ya somo hili	
Dakika 10 **Kabla ya majadiliano**	**Kutayarisha/Tengeneza Maduara** Elezea kuhusu mbinu za ufundishaji za Sokratesi kwa walimu. Tumia maelezo yaliyotayarishwa kwenye projekta au yaliyoandikwa kwenye chati. Waongoze washiriki kujadili maduara ya Sokratesi ambayo yanahimiza kila mshiriki kusema kwa uwazi mawazo yake. Wagawe washiriki katika vikundi vya watu 4-6 kulingana na ukubwa wa chumba cha mafunzo na wingi wa washiriki. Wape washiriki swali litakaoongoza	**Panga** Walimu wasikilize maelezo ya mbinu za ufundishaji za Sokratesi na kuchunguza maelezo hayo. Walimu wajipange katika vikundi vya washiriki 4-6 Walimu wasikilize jinsi ya kujadiliana katika maduara ya Sokratesi: *Kila mshiriki atasoma tafakari yake kwa wenzake katika kikundi. Washiriki wengine wasikilize bila kuingilia kati kutoa maoni. Baada ya kila mshiriki kusoma uzoefu wake mbele ya kikundi, washiriki wote wajadiliane kile walichosikia kutoka*

	majadiliano	*kwa wenzao walipokuwa wanasoma. Hakuna kanuni katika majadiliano haya. Bali taja chochote ulichosikia kikisomwa na wenzako.*
Dakika 60 **Wakati wa majadiliano**	**Kufuatilia** Fuatilia mijadala katika makundi, usitathimini wala kusahihisha majadiliano yao. Bali kusanya taarifa kuhusu kile wanachojadiliana. Kama kikundi kimekwama na kukaa kimya, kaa nao na waulize maswali ya kuwaongoza ili majadiliano yaendelee. Kisha ondoka.	**Kujadiliana** Walimu watumie swali la kuwaongoza kufungua majadiliano ya wazi kuhusu jinsi wanavyofundisha Usomaji.
Dakika 10 **Baada ya majadiliano**	**Mrejesho** Toa mrejesho usiorasmi kwa washiriki. *Hivi ndivyo vitu nilivyosikia katika majadiliano yenu leo:* Taja maeneo ya ufundishaji bora na ufundishaji dhaifu waliyojadili na kuyasema. Nia ya zoezi hili ni kumsaidia mwalimu aseme pale wanapofanya vizuri katika ufundishaji wake na pale wanapohitaji kupafanyia kazi zaidi na kile nachohitaji kufanya bila kuhukumiwa.	**Kutafakari** Walimu wasikilize mrejesho na kutoa maoni yao ya mwisho kuhusu mchakato na maudhui ya maduara ya Sokratesi.

Somo la 3: Kujenga Usuli wa Maarifa (Dakika 120)

Vifaa: Kitini cha Kusoma kwa Ufahamu, vifaa vya kuandikia, chati na kalamu ya wino mzito

Malengo ya somo: Mwalimu aweze:

1. Kujadili kwa kina vipengele vyote vitano vya usomaji
2. Kufafanua ufasaha kwa usahihi, kama matokeo ya ufundishaji bora wa stadi za Usomaji na siyo kufundisha ufasaha kama stadi
3. Kueleza umuhimu wa kufundisha Kusoma kwa Ufahamu kwa walengwa kama msingi wa kujenga uwezo wao wa kusoma
4. Kutaja njia mbalimbali za kufundisha Kusoma kwa Ufahamu

Muda	**Shughuli ya Mwezeshaji**	**Shughuli za Mwalimu**
Dakika 5 **Utangulizi**	**Kuanzisha somo:** Mwezeshaji elezea kuhusu: **Mada –** Usuli wa Maarifa ya Usomaji **Shughuli –** Kusoma, kuandika, kubainisha taarifa muhimu, Elezea malengo ya somo hili	
Dakika 15 **Kabla ya Kusoma**	**Maelezo ya awali Kabla ya Kusoma** Waambie walimu kuwa watajifunza na kusoma zaidi kuhusu jinsi ya kufundisha usomaji katika somo hili. Waambie kuwa ingawa vipengele vyote vitano vya usomaji ni vya muhimu, somo hili linawachagiza walimu na mawazo matatu mapya ambayo ni: 1. *Ufasaha siyo ufundishaji mzuri, bali ufasaha ni matokeo ya ufundishaji mzuri wa kusoma.* 2. *Kufundisha Kusoma kwa Ufahamu ni kitu chenye umuhimu wa juu anachopaswa kufanya mwalimu anayefundisha kusoma.* 3. *Kuwataka wanafunzi wasome kwa sauti, hakuwasaidii kuelewa matini wanayosoma, ila kusoma kimya kunawafanya kuelewa matini wanayosoma.* Waambie walimu waeleze kama wanakubaliana au hawakubaliani na	**Kujitayarisha Kusoma** Walimu wajibu kuhusu mawazo makuu matatu kwa kuinua mikono yao Katika kitini cha Kusoma kwa Ufahamu walimu wasome matini waliyopewa kwa kuweka alama

	maelezo hayo hapo juu kabla ya kusoma katika kitini. Pata idadi ya wanaokubaliana na wale wasiokubaliana Tayarisha mchakato wa kusoma kwa kubainisha matini na maelekezo ya kusoma kwa kuweka alama katika matini: **!** *Ni taarifa muhimu kukumbuka* **?** *Swali/nahitaji ufafanuzi* **+** *Jinsi gani ya kufanya/nahitaji kujifunza zaidi* Tumia wasilisho katika projekta au andika kwenye chati.	
Dakika 40 **Wakati wa kusoma**	**Kuwezesha** Tembea na chunguza kama kuna washiriki wanahitaji msaada. Wakumbushe kuhusu muda wao wa kusoma zikibaki dakika 20, halafu dakika 5	**Kujifunza** Wasome matini katika kitini cha Kusoma kwa Ufahamu (kuhusu usomaji hadi mbinu za uomaji endelevu) Watumie alama katika matini **!** *Ni taarifa muhimu kukumbuka* **?** *Swali/nahitaji ufafanuzi* **+** *Jinsi gani ya kufanya/nahitaji kujifunza zaidi*
Dakika 30 **Baada ya Kusoma**	**Kutathmini Ujifunzaji** Wezesha majadiliano katika kundi kubwa. Anza na maswali yaliyojitokeza, Kisha taarifa muhimu walizoona na mwisho mambo wanayotaka kujifunza zaidi Chukua idadi ya wale wanaokubaliana na wasiokubaliana baada ya kusoma matini.	**Kutafakari/KuJadiliana** Walimu washiriki katika majadiliano katika vikundi Walimu washiriki katika zoezi la pili kuona kama bado wanakubaliana au hawakubaliani au wamebadilika Walimu watoa maoni ya kuhitimisha kama wanayo

Somo la 4: Misingi ya Ufundishaji wa Kusoma kwa Ufahamu (Dakika 90)

Vifaa: Madaftari ya kuandikia, chati, makapeni.

Malengo ya somo: Mwalimu aweze:

1. Kubainisha aina mbili za masomo ya Kusoma kwa Ufahamu
2. Kuelezea muundo wa kabla/wakati wa/baada ya kusoma
3. Kutambua nini cha kufanya na nini kisifanyike wakati wa ufundishaji wa Kusoma kwa Ufahamu

Muda	Shughuli ya Mwezeshaji	Shughuli za Mwalimu
Dakika 5 **Utangulizi**	**Kuanzisha Somo**: Mwezeshaji elezea kuhusu: **Mada** – Misingi ya Kusoma kwa Ufahamu **Shughuli –** Kutafakari, kusoma, kuandika na majadiliano Elezea malengo ya somo hili	
Dakika15 **Kabla**	**Kutayarisha Jukwaa la Kusoma** Waambie walimu watafakari na kisha andika tafakuri zao kwenye chati Wape changamoto walimu kuandika mawazo yao ya sasa wakati wanapokuwa wanasoma matini. Waambie kuwa watapitia mawazo yao mwisho wa siku	**Kutafakari/Kujadiliana** Tafakari juu ya swali hili: *Fikiria kuhusu kipande cha matini ulichosoma na kujadili sasa hivi. Kutokana na taarifa hii uliyosoma, unafikiria Misingi ya Kufundisha Kusoma kwa Ufahamu inapaswa kuzingatia mambo gani?*
Dakika 40 **Wakati**	**Kuwezesha** Tembea na chunguza kama kuna washiriki wanahitaji msaada. Wakumbushe kuhusu muda wao wa kusoma zikibaki dakika 20, halafu dakika 5	**Kujifunze** Kwa kutumia chati ya pande mbili, walimu wasome katika mwongozo kuhusu misingi ya kufundisha Kusoma kwa Ufahamu mpaka vitu gani vya kufanya na vitu gani visifanyike wakati wa kufundisha Kusoma kwa Ufahamu
Dakika 30 **Baada**	**Kutathmini Ujifunzaji** Waombe walimu kushirikishana kile walichoandika katika chati ya pande mbili walipokuwa wanasoma. Kisha waulize kama wana maswali kuhusu usomaji.	**Kutafakari/Kujadiliana** Walimu washirikishane mambo muhimu waliyoyaona. Waulize maswali kuhusu usomaji.

Somo la 5: Mhutasari na Kushirikishana Tulichojifunza (Dakika 30)

Vifaa: Majarida, madaftari ya kuandikia, vifaa vya kuandikia chati, makapeni.

Malengo ya somo: Mwalimu atafakari:

1. Kuhusu kile walichojifunza kuhusu Kufudisha Usomaji kwa Ujumla
2. Kuhusu kile walichojifunza mahususi kuhusu Kufundisha Kusoma kwa Ufahamu
3. Jinsi fikira na mawazo yao yalivyokua na kubadilika siku ya leo kuhusu Usomaji

Muda	**Shughuli ya Mwezeshaji**	**Shughuli za Mwalimu**
Dakika 2 **Utangulizi**	**Kuanzisha Somo**: Mwezeshaji elezea kuhusu: **Mada** – Kushirikishana Tulichojifunza **Shughuli –** Kutafakari, njozi za washiriki Elezea malengo ya somo hili	
Dakika 5 **Kabla ya Kuandika**	**Kutayarisha Mchakato wa Kuandika** Waambie walimu watafakari jinsi siku ilivyoanza. Waombe wasome tena kile walichoandika mwanzo wa siku kuhusu ufundishaji wao wa kusoma. Waombe sasa waandike tena kwa ufupi jinsi watakavyofundisha somo la Kusoma kwa Ufahamu kuanzia sasa. Waambie watashirikishana maelezo yao na wenzao mezani pindi wakimaliza kuandika.	**Kujitayarisha Kuandika** Walimu wasome tena kile walichoandika wakati siku ilipoanza na wajiandae kuandika tena kwa ufupi.
Dakika 10 **Wakati wa Kuandika**	**Kuwezesha** Tembea darasani na himiza walimu wale wanaoangaika kuandika njozi zao.	**Kutafakari** Andika njozi yako mpya kuhusu kufundisha Kusoma kwa Ufahamu darasani.
Dakika 12 **Baada ya Kuandika**	**Kuwezesha** Waombe walimu wasome kile walichoandika kwa wenzao katika meza zao. Waambie kuwa hivyo tunavyomaliza siku ya leo. na wakimaliza kusoma njozi zao kwa kila moja. Waagane mpaka kesho yake. Mbinu hii inaitwa *"Kusoma Nje ya Chumba"* inalenga kumaliza siku.	**Kutafakari /Kujadiliana** Kila mwalimu asome njozi yake mpya ya kufundisha Kusoma kwa Ufahamu kwa mwenzake

SIKU YA 2

Somo la 6: Kuchunguza Sampuli za Masomo (Dakika 90)

Vifaa: Kitini cha Kusoma kwa Ufahamu, majarida, karatasi kubwa za chati, kalamu za makapeni, na daftari la kuandikia

Malengo ya somo: Mwalimu aweze:

1. Kuelezea muundo wa somo la Kusoma kwa Ufahamu
2. Kutaja sampuli za masomo
3. Kujadiliana na wengine

Muda	Shughuli ya Mwezeshaji	Shughuli za Mwalimu
Dakika 5 **Utangulizi**	**Kuanzisha Somo**: Mwezeshaji elezea kuhusu: **Mada** – Sampuli za Masomo **Shughuli –** Kujifunza katika Jozi/ kumfundisha mwenzako Elezea malengo ya somo hili	
Dakika 10 **Kabla ya kujadiliana**	**Kuwezesha** Waambie walimu kuwa watakuwa wanaangalia sampuli za masomo ili kuwasaidia katika kuandaa masomo ya Kusoma kwa Ufahamu Waambie kuwa watachunguza sampuli 2 za masomo zilizounganishwa pamoja: 1) somo ambalo mwalimu anaonyesha jinsi na 2) somo linalomlenga mwanafunzi mwenyewe Kusoma kwa Ufahamu Waombe walimu kukaa katika jozi za washiriki kulingana na umri wa wanafunzi wanaowafundisha yaani: 1) Wasomaji wa ngazi ya awali; 2) Wasomaji wa ngazi ya kati; na 3) Wasomaji wa ngazi ya juu Waambie watajifunza kwa pamoja na baadaye watawafundisha wenzao walichokuwa wanajifunza (kufundishana wao kwa wao). Kwa	**Kujitayarisha Kujifunza katika Jozi** Walimu kugawanyika katika jozi za washiriki kulingana na umri wa wanafunzi wanaowafundisha yaani: 1) Wasomaji wa ngazi ya awali; 2) Wasomaji wa ngazi ya kati; na 3) Wasomaji wa ngazi ya juu Walimu watabaki katika jozi hizi muda wote. Walimu wafunue kitini cha mafunzo kwenye viambatisho kwa ajili ya masomo yao mawili watakayo tayarisha na kuyatumia katika ufundishaji kiduchu.

	hiyo watahitaji; 1) kusoma na kujadadiliana; 2) kujitayarisha kuwafundisha wenzao kuhusu somo hili	
Dakika 30 **Wakati wa majadiliano**	**Kuwezesha** Tembea tembea ndani ya darasa kuhakikisha kuwa jozi zinafahamu kile wanachotakiwa kufanya. Wakumbushe kuwa watatakiwa kuwafundisha wenzao wakimaliza.	**Kujifunza** Jozi za washiriki zijifunze masomo ya kusoma yote mawili na kujitayarisha kwa ufundishaji kiduchu kisha wawaeleze wenzao mambo muhimu kuhusu kila somo
Dakika 50 **Baada ya majadiliano**	**Kuwezesha** Tayarisha na wezesha mchakato wa kufundishana (dakika 10). Wajibu wako ni kutunza muda. Kila jozi ya washiriki itumie muda wa dakika 12 kufundisha wenzao masomo yote 2	**Kufundishana** Jozi za washiriki zitengeneze vikundi 6 vya 1) Wasomaji wa ngazi ya awali; 2) Wasomaji wa ngazi ya kati; na 3) Wasomaji wa ngazi ya juu. Kila kikundi kiwe na uwakilishi wa aina zote tatu za wasomaji ili masomo yote sita yafundishwe kiduchu katika kila kikundi. Kila jozi ifundishe kiduchu masomo yote mawili waliyoyafanyia kazi

Somo la 7: Kutayarisha Masomo Mawili Yaliyounganika Pamoja (Dakika 90)

Vifaa: Kitini cha Kusoma kwa Ufahamu, sampuli za masomo, kifani tupu cha jinsi ya kuandaa somo (vifani 3 kwa kila mshiriki)

Malengoya somo: Mwalimu aweze:

1. Kutumia kifani cha kuandaa somo kutayarisha masomo mawili wanayoweza kuyatumia darasani na wanafunzi wao

Muda	Shughuli ya Mwezeshaji	Shughuli za Mwalimu
Dakika 5 **Utangulizi**	**Kuanzisha Somo**: Mwezeshaji elezea kuhusu: **Mada** – Kutayarisha masomo **Shughuli –** Kufanya kazi za kutayarisha masomo Elezea malengo ya somo hili	
Dakika 10 **Kabla kuandaa masomo**	**Kutayarisha Jukwaa** Waambie walimu kuwa watachagua kitabu kimojawapo watakachotumia kuandaa masomo mawili yaliyounganika: 1) somo ambalo mwalimu anaonyesha jinsi na 2) somo linalomlenga mwanafunzi mwenyewe Kusoma kwa Ufahamu Waambie kuwa wanaweza kufanya kazi pekee yao au wawili. Wape kifani kitupu cha kuandaa somo	**Kujitayarisha kupanga** Walimu watumie vitabu vilivyopo kutayarisha masomo mawili yaliyounganika pamoja. Wafanye kazi ya kutayarisha masomo haya pekee yao au katika jozi zao
Dakika 60 **Wakati wa kuandaa masomo**	**Kuwezesha** Tembea tembea darasani ukiwasaidia walimu kuandaa masomo	**Kuandaa** Walimu waandae masomo
Dakika 15 **Baada kuandaa masomo**	**Kuwezesha** Waulize walimu jinsi mchakato wa kuandaa somo ulivyokwenda. Waombe walimu watoe maoni yao na waulize maswali waliyonayo. Jadili na kujibu maswali yao inavyopaswa	**Kutafakari/Kujadiliana** Walimu wajadiliane na kuuliza maswali

Somo la 8: Kufundisha Wenzako Somo (Dakika 120)

Vifaa: Vitabu, masomo yaliyoandaliwa na walimu wenyewe

Malengo ya Somo: Mwalimu aweze:

1. Kufundisha wenzao kile walichokiandaa
2. Kujenga uzoefu wa kuandaa masomo ya Kusoma kwa Ufahamu

Muda	Shughuli ya Mwezeshaji	Shughuli za Mwalimu
Dakika 5 **Kabla**	**Kuanzisha Somo**: Mwezeshaji elezea kuhusu: **Mada –** Kufundisha wenzako somo kiduchu **Shughuli –** Kufanya mazoezi ya kufundishana katika vikundi vidogo Elezea malengo ya somo hili	
Dakika 35 **Wakati**	**Kuwezesha** Waambie walimu kuwa watakuwa na dakika 35 za kuchagua na kuandaa somo moja kati ya mawili waliyoandaa	**Kujiandaa** Walimu wachague somo moja , walipitie na kufanya mazoezi ya kufundisha wenzao
Dakika 80 **Baada**	**Kuaathmini Ujifunzaji** Wagawe walimu katika vikundi vya washiriki wanne siyo kubwa zaidi ya hao. Waambie kuwa kila moja ana dakika 20 za kuonyesha jinsi ya kufundisha Waambie kuwa wana dakika 15 za kuonyesha jinsi wanavyofundisha na dakika 5 za kupata mrejesho toka kwa wenzao. Chunga muda wao	**Kuonyesha Jinsi** Walimu wafundishe masomo kwa wenzao katika vikundi vyao vya watu wannw Kila moja ana dakika 20 za kufundisha wenzake watatu. Dakika 15 za kufundisha na dakika 5 za kupata mrejesho kutoka kwa wengine.

Somo la 9: Kufunga (Dakika 30)

Muda	Shughuli ya Mwezeshaji	Shughuli za Mwalimu
Dakika 5 **Utangulizi**	**Kuanzisha Somo**: Mwezeshaji elezea kuhusu: **Mada** – Kufunga **Shughuli –** Kutafakari na kutathmini Elezea malengo ya somo hili	
Dakika 10 **Kabla**	**Kuchunguza Maarifa** Waulize washiriki kueleza walichojifunza (dakika 5) Andika walichojifunza toka kila meza (dakika 5)	**Kutafakari/kujadili** Walimu watafakari kile walichojifunza
Dakika 10 **Wakati**	**Kuwezesha** Watake walimu kufanya Azimio moja kila mmoja la kufundisha Kusoma kwa Ufahamu kwa kutumia njia mpya. Watake walimu kuandika maazimio yao katika kadi na wayakusanye.	**Azimio** Walimu waandike maazimio yao kwenye kadi
Dakika 5 **Baada**	**Kutathmini Mafunzo** Waombe walimu wajaze fomu ya kutathmini mafunzo na zikusanye	**Kutafakari/Kujadiliana** Walimu wajaze fomu ya kutathmni mafunzo na kuzikusanya